Find this and other free resources at https://maktaba.tetea.org

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

MTIHANI WA TAIFA WA DARASA LA NNE - 2012

054 **SOMO: KISWAHILI**

JINA LA MTAHINIWA: .....

JINA LA SHULE: .....

HALMASHAURI: .....

MKOA: .....

MUDA: SAA 1

MAELEKEZO:

1. Mtihani huu una sehemu tano A, B, C, D, na E zenye jumla ya maswali 25.
2. Majibu ya maswali yote yaandikwe kwenye karatasi za mtihani huu.
3. Kumbuka kuandika jina lako, jina la shule, halmashauri na mkoa.
4. Simu za mkononi haziruhusiwi kwenye chumba cha mtihani.

Find this and other free educational resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

Find this and other free resources at https://maktaba.tetea.org

SEHEMU: A

IMLA

Sikiliza kwa makini kisha uandike sentensi zitakazosomwa na msimamizi wa mtihani kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi:

1. .....
2. .....
3. .....
4. .....
5. .....

SEHEMU: B

Jibu swali la 6 - 10 kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku.

6. Nini maana ya kutia nanga?
   A. Kutia uzito jambo
   B. Kufika mwisho wa jambo
   C. Kuanza kutenda jambo
   D. Kuzorotesha jambo

7. Mvungu ni sehemu ya .....
   A. Kando ya kitanda
   B. Mbele ya kitanda
   C. Juu ya kitanda
   D. Chini ya kitanda

8. ..... mama yangu alipopona malaria.
   A. Ningefarijika
   B. Nitafarijika
   C. Ninafarijika
   D. Nilifarijika

9. Kwa kawaida jua huzama upande wa .....
   A. Kusini
   B. Kaskazini
   C. Magharibi
   D. Mashariki

Find this and other free educational resources at:
https://maktaba.tetea.org
Scanned with CamScanner

Find this and other free resources at https://maktaba.tetea.org

10. ..... wasiofuata sheria za barabarani husababisha ajali.

A. Marubani

B. Manahodha

C. Madereva

D. Maboharia

SEHEMU: C

Jibu swali la 11 – 15 kwa kuchagua maneno katika kisanduku ulichopewa

anabudi, huhisi, mchuzi, donda, hanabudi, kidonda, mchukuzi, alikwenda, husikia, tende, hakwenda

11. Mdharau mwiba mguu huota .....

12. Amina ..... kununua mkate kwa kuwa hakuwa na fedha.

13. Ili afanikiwe katika masomo ..... kusoma kwa bidii.

14. Kuvuja kwa pakacha nafuu kwa .....

15. Majira ya kipupwe watu ..... baridi.

SEHEMU: D

Jibu swali la 16 – 20 kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi

16. Andika wingi wa neno busara .....

17. Asha ..... Ali wamefanana sana.

18. Paa ni sehemu ya ..... ya nyumba

19. Hakimu husikiliza kesi za watuhumiwa mahali gani? .....

20. Nauli ya ndege ni kubwa ..... ya basi.

SEHEMU: E

Soma shairi lifuatalo kisha soma swali la 21 – 25 kwa kuchagua herufi ya jibu lililo sahihi

Ikiwa hujafahamu,
Alosomesha mwalimu,
Usione ugumu,
Mkono kuunyanyua.

Unapofika nyumbani ,
Daftari mkononi,
Durusu ya darasani,
Kichwani yapate kaa.

Find this and other free educational resources at:
https://maktaba.tetea.org
Scanned with CamScanner

Find this and other free resources at https://maktaba.tetea.org

Walipunguza kucheza,
Kwa ari wakajifunza,
Ndiyo leo wakaweza,
Umma kuutumikia.

21. Mtunzi wa shairi anashauri kuwa kama mwanafunzi hajaelewa jambo anapaswa .....
    A. Kujisomea daftarini
    B. Kuuliza swali kwa mwalimu
    C. Kujisomea kitabuni
    D. Kuuliza swali kwa mwanafunzi.

22. Mwanafunzi anapofika nyumbani kutoka shuleni anashauriwa
    A. Kushika daftari mkononi
    B. Kuwaeleza wazazi aliyojifunza
    C. Kurudia kusoma aliyojifunza
    D. Kupumzika kwa kuwa amechoka

23. Neno "ari" katika shairi hili limetumika kwa maana ya .....
    A. Juhudi
    B. Akili
    C. Busara
    D. Werevu

24. Mshairi anabainisha kuwa athari ya kucheza sana darasani ni .....
    A. Kuelewa sana
    B. Kupata afya njema
    C. Kuumia michezoni
    D. Kushindwa kujifunza vizuri

25. Kichwa cha habari kinachofaa shairi hili ni nini?
    A. Elimu
    B. Durusu
    C. Umma
    D. Walimu

Find this and other free educational resources at:
https://maktaba.tetea.org
Scanned with CamScanner